**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**


Anwani ya Simu **"REGCOM"**
Simu: 2545608/2545820/2545872
Fax: 2545239/2544386
Unapojibu tafadhali taja
Kumb.Na.FA.7/257.02"A"

OFISI YA MKUU WA MKOA,
P.O. BOX 3050,
**ARUSHA,**


**16/11/2021**

# MKATABA WA UTOAJI HUDUMA YA UKARABATI WA ICU NA EMD MT. MERU HOSPITALI.

Namba ya Mkataba: **ME/007/MTMERU RRH/2021-22/W/6/LOT1**

Mkataba huu umefanyika leo tarehe **16 Mwezi 11 Mwaka, 2021**.

*KATI YA*

**KATIBU TAWALA MKOA-ARUSHA S.L.P** 3050 ARUSHA **ambaye** ni Mwajiri/Afisa Masuhuli.

**NA**

**GODWIN H. SHOO** ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama mtoa huduma/Local Fundi kwa upande wa pili.

Kwa kuwa Mganga mfawidhi wa hospitali (Mt Meru) anatarajia kufanya kazi ya **UKARABATI WA ICU NA EMD MT. MERU HOSPITALI.** ambapo chanzo cha fedha ni **SERIKALI KUU.**

Kama mtoa huduma/Local Fundi **GODWIN H. SHOO** nimekubali kutoa huduma hiyo kwa muda wa siku 90 kuanzia tarehe nitakayokabidhiwa eneo la kazi.

**HIVYO PANDE ZOTE MBILI WANAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO;**

1. Kwamba Mkataba huu utakuwa ni wa kiasi cha Shilingi za Kitanzania Tzs. **57,420,000** (million hamsini na saba elfu laki nne na elfu ishirini tu),**ikiwa ni gharama za huduma ya ukarabati wa icu na emd mt meru hospitali**
2. **Mkataba huu unategemea kuanza rasmi mara baada ya kupokea barua kutoka kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya rufaa ya Mt Meru-ARUSHA.**
3. Utekelezaji wa **UJENZI** huu utafanyika mara moja na local fundi kwa kuzingatia ramani, ***"BOQ"*** na maelekezo yote yatakayotolewa na Mhandisi wa ujenzi kwa niaba ya Afisa masuhuli na kamati ya ujenzi.
   - Fundi atatakiwa kufanya kazi zote zinazohusika na kazi za ujenzi kwa awamu husika, ikiwa ni Pamoja na kufanya umwagiliaji wa maji katika zege, matofali, na kazi zinginezo.
4. Fundi atakuwa na wajibu wa kuweka mtaalamu au yeye mwenyewe kusimamia kazi za ujenzi wakati wote kazi zinaendelea eneo la ujenzi, na pia atatakiwa kufanya kazi kwa weledi na kuhakikisha anazingatia ubora na viwango vya kazi
5. Fundi wakati wote awapo eneo la kazi atapaswa kuzingatia sheria za nchi na kanuni za ujenzi ikiwa ni pamoja na kuwa na mavazi na vifaa vya kujikinga na ajali(protective gears)wakati wote fundi anapokuwa katika kazi za ujenzi
6. Kwamba mwajiri anaweza kusitisha mkataba huu wakati wowote endapo kutakuwa na kukiukwa kwa masharti ya mkataba.
7. Kwamba malipo yatafanyika kwa kuzingatia kazi zitakazo kaguliwa na karani na baada ya fundi kuwasilisha barua ya maombi ya malipo na Mhandisi kuhakiki kazi husika. **(Valuation of works)** na kutoa cheti ***"certificate"***
8. Kwamba mkataba huu utakuwa ni wa siku **90** kuanzia tarehe ya kukabidhiwa eneo la mradi.
9. Kwa makubaliano haya na masharti yote yaliyoainishwa na kukubaliwa na pande zote mbili yanakamilisha mkataba huu.

**MKATABA UNASAININIWA NA KUWEKWA MUHURI WA KATIBU TAWALA MKOA:**

**Jina** Dkt. Athumani J. Kihamia

**Saini** ……………[signature]……………

**Tarehe** 16.11.2021

**MBELE YA;**
**Jina :** DKT ALEX ERNEST

**Sahihi ;**……………[signature]……………

**Cheo :** TMO1/C

MGANGA MFAWIDHI WA HOSPITALI
S.L.P 3092
ARUSHA
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA ARUSHA

**KWA UPANDE WA MTOA HUDUMA**

**UMETIWA SAINI NA:**

**Jina** GODWIN H. SHOO

**Saini** ……………[signature]……………

**Tarehe** 16.11.2021

**MBELE YA**

**Jina** WILFREA G. TEMBA

**Saini** Temba

**Tarehe** 16.11.2021